

# Jinsi ya kujiandikisha kupiga kura

Mwongozo rahisi wa kusoma




# Enrol

---

---

---

---



## Jinsi ya kutumia mwongozo huu



Tume ya Uchaguzi ya Australia (AEC) iliandika mwongozo huu. Wakati unapona neno 'sisi', linamaanisha AEC.



Tumeandika mwongozo huu kwa njia rahisi ya kusoma.

Tunatumia picha kueleza mawazo mengine.



Tumeandika maneno kadhaa kwa **herufi nzito**.

Tunaeleza maana ya maneno haya. Kuna orodha ya maneno haya kwenye ukurasa 16.



Unaweza kuomba msaada wa kusoma mwongozo huu. Rafiki, mtu wa familia au mtu msaidizi anaweza kukusaidia.

## Ni nini katika mwongozo huu?

Kupiga kura katika uchaguzi	4
Kuandikisha kupiga kura	6
Nini kitafuata?	12
Nini ikiwa utahama nyumba?	13
Je! Upo tayari kwenye rejesta ya wapiga kura?	14
Unawezaje kupata habari zaidi?	15
Orodha ya maneno	16
Wasiliana nasi	17


## Kupiga kura katika uchaguzi



Hapa Australia tuna **uchaguzi wa serikali ya shirikisho** karibu kila miaka 3.



Uchaguzi wa shirikisho ni kwa nchi nzima.



Ni jinsi tunavyochagua serikali ya Australia.



Gavana Mkuu anachagua tarehe ya uchaguzi.

Siku ya uchaguzi itakuwa Jumamosi.



Siku hiyo, watu wa Australia **watapiga kura**.

Wakati unapopiga kura, unasaidia kuchagua ni nani ambao ni sehemu ya serikali ya Australia.



Unapaswa kupiga kura ikiwa wewe:

- ni **raia** wa Australia na
- una umri wa miaka 18 au zaidi.



Raia ni mtu anayepewa haki na uhuru wa nchi anapoishi.



Kupiga kura kunakupa nafasi kutoa maoni yako juu ya nani wataongoza nchi yetu.



Usijali kama hujapiga kura hapo awali.




Tunaeleza unachohitaji kufanya.

## Kuandikisha kupiga kura



Kabla ya kupiga kura, unapaswa **kujiandikisha**.



Unapojiandikisha, tunasajili jina lako kwenye orodha ya **wapiga kura** – yaani, watu ambao wanaweza kupiga kura.

Orodha hii inaitwa **rejesta ya wapiga kura**.



Ili kusajili jina lako kwenye rejesta ya wapiga kura, unapaswa kujaza fomu ya kuandikisha.

**18+**



Ikiwa wewe ni karibu miaka 18, unaweza kujiandikisha sasa.

Unapofika miaka 18, utakuwa tayari kupiga kura.



Unaweza kujaza fomu ya kuandikisha:

- mtandaoni
- kwenye karatasi.



Unaweza kujiandikisha kupiga kura wakati wowote.

Lakini unapaswa kujiandikisha kabla rejesta ya wapiga kura kufungwa ili kupiga kura katika uchaguzi.



Rejesta ya wapiga kura hufungwa wiki 1 baada ya Gavana Mkuu kuchagua tarehe ya uchaguzi.



Ikiwa utajiandikisha kabla rejesta ya wapiga kura kufungwa, hutakosa.

## Kuandikisha mtandaoni



Unaweza kutembelea tovuti yetu ili kuandikisha kupiga kura mtandaoni.

[www.aec.gov.au/enrol](http://www.aec.gov.au/enrol)

Kuna kitufe kinachosema: Enrol online (Jiandikisha mtandaoni).



Unahitaji kujibu maswali kadhaa.



Utaulizwa kwa uthibitisho wa wewe ni nani, kama vile:

- leseni ya dereva
- pasipoti.



Mtu mwingine kwenye rejesta ya wapiga kura pia anaweza kuthibitisha kuwa anakujua.



Ikiwa unataka, unaweza kuuliza mtu kukusaidia.



Unapomaliza, unahitaji kutumia kitufe kinachosema: Submit (Peleka).



## Kuandikisha kwenye karatasi



Ili kujiandikisha kwenye karatasi, unahitaji kujaza fomu ya kuandikisha.



Unaweza kupata fomu ya kuandikisha katika ofisi yoyote ya AEC.



Ikiwa unatupigia simu, tunaweza kukutumia fomu ya kuandikisha katika posta.

Nambari yetu ya simu ni **13 23 26**.



Unahitaji kujibu maswali kadhaa.



Utaulizwa kwa uthibitisho wa wewe ni nani, kama vile:


- leseni ya dereva
- pasipoti.



Mtu mwingine kwenye rejesta ya wapiga kura pia anaweza kuthibitisha kuwa anakujua.




Ikiwa unataka, unaweza kuuliza mtu kukusaidia.



Unapomaliza, unahitaji kututumia fomu.

Unaweza:




- Kuituma kwetu:

AEC

Reply Paid 9867

Katika mji mkuu wako


Hakuna haja kutumia stempu.



- ichukue kwa ofisi ya AEC

Ikiwa utatupigia simu, tunaweza kukusaidia kupata ofisi ya AEC karibu nawe.

**13 23 26**



- ichanganue na kuipakia kwenye tovuti yetu.

[www.aec.gov.au/return](http://www.aec.gov.au/return)

## Nini kitafuata?



Wiki chache baada ya kujiandikisha, tutakutumia barua.




Barua itasema kuwa jina lako limeongezwa kwenye rejesta ya wapiga kura.



Hii inamaanisha unaweza kupiga kura katika uchaguzi wa shirikisho.

## Nini ikiwa utahama nyumba?



Unahitaji kutuambia kila wakati unapohama.



Hii inatusaidia kusasisha rejesta ya wapiga kura kuwa mpya.



Ikiwa unahamia nyumba mpya, tafadhali jaza fomu mpya ya kuandikisha.

## Je! Upo tayari kwenye rejesta ya wapiga kura?



Ni rahisi kuangalia kama jina lako lipo kwenye rejesta ya wapiga kura.

Unaweza:



- tembelea tovuti yetu  
[www.aec.gov.au/check](http://www.aec.gov.au/check)



- utupige simu na tutaangalia kwa ajili yako  
**13 23 26**



- tembelea ofisi ya AEC na tutaangalia kwa ajili yako.

## Unawezaje kupata habari zaidi?



Ikiwa unataka kujua zaidi kuhusu kupiga kura, tuna miongozo 2 mingine ambayo unaweza kusoma:

- *Jinsi ya kupiga kura kwa mahali pa kupigia kura*
- *Jinsi ya kupiga kura kwa posta.*



Unaweza kupata miongozo hii kwenye tovuti yetu.

[www.aec.gov.au/assistance](http://www.aec.gov.au/assistance)

नमस्ते



Pia tuna habari kwenye tovuti yetu kwa watu wanaosema lugha zingine nje ya Kiingereza.

## Orodha ya maneno



### **Raia**

Raia ni mtu anayepewa haki na uhuru wa nchi anapoishi.



### **Rejesta ya wapiga kura**

Orodha ya wapiga kura.



### **Kuandikisha**

Wakati unapojiandikisha, tunaweka jina lako kwenye orodha ya wapiga kura.



### **Uchaguzi wa serikali ya shirikisho**

Uchaguzi wa shirikisho ni kwa nchi nzima. Ni jinsi tunavyochagua serikali ya Australia.



### **Kupiga kura**

Wakati unapopiga kura, unasaidia kuchagua ni nani ambao ni sehemu ya serikali ya Australia.



### **Wapiga kura**

Watu ambao wanaweza kupiga kura.



## Wasiliana nasi

Huduma ya Kitaifa ya Kupeleka Ujumbe (NRS)



Watumiaji wa TTY:

- Simu 13 36 77
- Uliza kwa 13 23 26



Watumiaji wa sema na sikiliza:

- Simu 1300 555 727
- Uliza kwa 13 23 26



Watumiaji wa Kupeleka Ujumbe Mtandaoni:

- Unganisha kwa NRS
- Uliza kwa 13 23 26



Lugha nyingine:

- Simu 1300 720 153



[www.aec.gov.au](http://www.aec.gov.au)



[/AusElectoralCom/](https://www.facebook.com/AusElectoralCom/)



[@AusElectoralCom](https://twitter.com/AusElectoralCom)



[@auselectoralcom](https://www.instagram.com/auselectoralcom)



Kikundi cha Kupata Habari kiliunda mwongozo huu rahisi ya kusoma kwa kutumia picha za hifadhi na picha maalum.

Picha hizo haziwezi kutumiwa tena bila ruhusa. Kwa maswali yoyote kuhusu picha, tafadhali tembelea

[www.informationaccessgroup.com](http://www.informationaccessgroup.com). Taja nambari ya kazi 3035-A.

Imeidhinishwa na Kamishna Naibu wa Uchaguzi, Kanberra.